TANGAZO LA SERIKALI NA. 221 la tarehe 28/3/2028

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA SHUGHULI ZA UVUVI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 276 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Shughuli za Uvuvi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Shughuli za Uvuvi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 4

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 4(2) kwa kuingiza maneno "kwa njia ya barua" katikati ya maneno "maombi" na "kwa".

Marekebisho ya kanuni ya 6

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 6(h) kwa kufuta neno "hawajapimwa" na badala yake kuweka maneno "hawajalipiwa ushuru".

Marekebisho ya kanuni ya 10

4. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 10 kwa-
(a) kufuta kanuni ndogo ya (2); na
(b) kubadili mpangilio wa kanuni ndogo ya (1) kuwa kanuni ya 10.

Kuongeza kanuni ya 10A

5. Kanuni Ndogo kuu inarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kanuni ya 10 kanuni mpya ifuatayo:

"Vyombo vya uvuvi visivyosajiliwa au vilivyojirudia namba

10A.-(1) Halmashauri au Wakala atakuwa na mamlaka ya kukamata vyombo vya uvuvi ambavyo havijasajiliwa au vimejirudia namba.

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kutaifisha na kuuza vyombo vilivyokamatwa chini ya kanuni ndogo ya (1), baada ya kupata idhini ya mahakama, iwapo havitasajiliwa ndani ya siku saba na fedha itakayopatikana italipia ada au ushuru anaodaiwa na kiasi kinachobakia atarudishiwa mmiliki.

(3) Wakala hataruhusiwa kutaifisha na kuuza au kufanya jambo lolote kwa vyombo vya uvuvi vilivyokamatwa bila kupata idhini ya Mkurugenzi.

(4) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa vyombo vya uvuvi vilivyokamatwa chini ya Sheria Ndogo hii isipokuwa tu kama ikithibitika kuwa uharibifu huo umesababishwa na Halmashauri au Wakala wake.".

Dodoma,
10 Januari, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi – OR-TAMISEMI*